# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA

**121/2**

## KISWAHILI 2

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **Alhamisi, 09 Mei 2019 asubuhi**

---

### Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenye jumla ya maswali **tisa (9)**.

2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka sehemu A, B, C na D. Katika sehemu E, swali la **tisa (9)** ni la lazima.

3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.

4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



f6may19
Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU A (Alama 20)

## FASIHI KWA UJUMLA

1. Uhakiki wa kazi za fasihi umejikita katika misingi ya fani na maudhui. Kwa kutumia kipengele cha mtindo, bainisha mambo sita yanayozingatiwa na wahakiki wa kazi za fasihi.

2. Fasihi ni chombo cha jamii kwa kuwa hushughulika na binadamu na ubinadamu wake. Kwa kutumia mifano, thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne.

## SEHEMU B (Alama 20)

## USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | **Haji Gora** |
| **Mapenzi Bora** | - | **Shabani Robert** |
| **Chungu Tamu** | - | **Theobald A. Mvungi** |
| **Fungate ya Uhuru** | - | **Mohamed S. Khatibu** |

3. "Kazi mojawapo ya fasihi andishi ni kupiga vita mambo yanayoweza kuzorotesha maendeleo katika jamii." Jadili kauli hii ukionesha na jinsi waandishi katika diwani mbili ulizosoma walivyotekeleza azma hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani.

4. Fafanua miundo ya mashairi katika diwani mbili ulizosoma kwa kuzingatia vipengele vitatu vya msingi vya muundo wa shairi.

## SEHEMU C (Alama 20)

## RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| **Usiku utakapokwisha** | - | **Mbunda Msokile** |
| **Kufikirika** | - | **Shabani Robert** |
| **Mfadhili** | - | **Hussein Tuwa** |
| **Vuta N'kuvute** | - | **Shafi Adam Shafi** |

5. Onesha namna dhamira za waandishi wa riwaya zinavyoonesha uhalisia wa Tanzania ya leo. Toa hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma.

6. Wasanii wa kazi za fasihi, hutumia methali na tamathali mbalimbali za semi kama zana za kutolea ujumbe uliokusudiwa. Bainisha methali tatu na tamathali za semi tatu kwa kila kitabu, kisha onesha jinsi zilivyotumiwa na waandishi wa riwaya mbili ulizosoma.



Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner

## SEHEMU D (Alama 20)

## TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - | **Ebrahim Hussein** |
| **Morani** | - | **Emmanuel Mbogo** |
| **Kivuli Kinaishi** | - | **Said Mohamed** |
| **Nguzo Mama** | - | **Penina Muhando** |

7. Waandishi wameonesha mambo yanayofaa na yasiyofaa kuigwa katika fasihi. Fafanua mambo mawili yanayofaa na mawili yasiyofaa kuigwa kama yalivyoainishwa na waandishi katika tamthiliya mbili ulizosoma.

8. Chagua wahusika wawili kati ya Chizi, Herbert, Mtolewa na Dongo, kisha fafanua wasifu wao ukilinganisha na wazo kuu la mwaandishi kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili ulizosoma.

## SEHEMU E (Alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

9. Soma matini ifuatayo kwa makini, kisha onesha mbinu za kifani zilizotumika.

Saa tatu usiku siku ya Jumamosi, niliamua kwenda kukaa katika baa moja maarufu mtaani kwetu iitwayo "WANYEJANDA" ili kupata moja moto moja baridi na nyama choma. Nilikaa meza moja peke yangu huku nikijisemea kimoyomoyo "Lenadi nimetulia katika ubora wangu." Pembeni ya meza yangu walikuwepo vijana watatu ambao kwa kweli walikuwa wamedorora na kuyumbayumba kutokana na kupiga maji kwa wingi. Kila mmoja alionekana akitazama chini huku midomo imetota uderere. Lakini hawakusahau mara kwa mara kuikusanya midomo hiyo wakijirejesha katika mazungumzo.

Wakati wakienda msalani kujisaidia, mmoja wa wale vijana waliokuwa wamekaa karibu na meza niliyokuwepo mimi alinisabahi kwa kuniambia;

Mambo vipi buroooo?

Poa! Nikamjibu.

Unatuchunia siyo, wajifanya hututambui?

Kwa mwanga hafifu uliokuwepo, tayari nilikuwa nimeshavaa miwani ya mbao. Haikuwa rahisi kuwatambua ni akina nani hao. Ikanipasa niwasogelee kwa karibu. "Aisee, ni wewe?" Ni mimi bwana, hunioni? Kweli ni wewe? Siamini! Amini bwana au umeshalewa? Alikuwa ni Masineki jirani yangu pale mtaani ninapoishi. Alikuwa pamoja na rafiki zake Mahewa na Kishefu. Ilinipasa kuwaomba msamaha ili kuyamaliza.


Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

Meza yao ilikuwa ikitazama matokeo ya chupa za pombe ambazo zilikuwa zimenuna. Siku hiyo nilikuwa na ukwasi wa kutosha na mkono wa birika kwangu ni haramu. Nilipapasa mfuko nikakuta umejaa mawe ya kutosha. Nilimwita mhudumu, "Oya mrembo wape kila mmoja kinywaji akipendacho!" "Thank you brother" Mahewa alisema. Kishefu alikuwa bado akitafakari jambo fulani, baadaye naye akasema "Burooo uko vizuri!" Wote tulitazamana tukakenua meno.

Ah...Ahaaaa...aaa! Dunia ni tamu jamani, ni tamu mno! Dunia ya sasa kila mtu anapambana na hali yake. Magumashi na madili siku hizi hakuna. Viongozi wapenda rushwa wapo roho juu wanajua siku yoyote kitanuka. Biashara haramu zimedhibitiwa kisawa sawa katika kila kona. Kweli "Dunia hadaa, ulimwengu shujaa." Nilimsikia Mahewa akisema.

Wakati wa ujana wetu, mimi baba yenu,
Shati dukani shilingi sita unapata!
Lakini sasa shilingi sita, hata mkate hupati!

*Kwa hiyo wanangu, tuishi kufuatana na wakati x2 (Kibwagizo)*

Jiepusheni na anasa, fanyeni kazi kwa bidii,
Kama kuna mkorofi kati yenu aache mara moja!

Hayo ni maneno ya mzee mmoja wa makamo aliyekuwa akiimba huku akiwanyanyua watoto wake alioongozana nao ili waondoke kurudi nyumbani baada ya kushibisha roho zao.

Myaaauu...myaaau.....myaaau! Sauti ya paka aliyekuwa uvunguni mwa meza ilisikika. Mara simu ikaita kutoka mfukoni mwa suruali yangu. Nilipoangalia alikuwa ni "wife" aliyenipigia akitaka nirudi nyumbani. Kwa jinsi nilivyomfahamu mke wangu huwa ni pilipili hasa ninapochelewa kurudi nyumbani; nilitii wito huo, hivyo mimi na Masineki tuliongozana njia moja kwa kuwa tulikuwa majirani. Kishefu na Mahewa waliamua kula kona kivyao kwa kuwa walikuwa na bodaboda yao.





Find more free educational resources at:
http://maktaba.tetea.org

Scanned by CamScanner